JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI-TANZANIA (TARURA)

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2015 /2020) KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI, 2019 HADI JANUARY, 2020

1. Utangulizi

Halmashauri ya Mji makambako in matandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 587.31. mtandao huo umegawanyika katika madaraja mbalimbali ya barabara kama jedwali na. 1 hapo chini linavyoonyesha

Jedwali Na. 1: Mtandao wa barabara katika halmashauri ya Mji wa Makambako.

Barabara za Mkusanyo (collector roads)	barabara za mlisho (feeder roads)	barabara za Mji (urban Roads)
km. 237.25	km. 133.22	km. 216.84

2. Hali ya upitikaji wa Barabara kwa mwaka

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Juni 2019 hadi January 2020 hali ya barabara za Halmashauri ya Mji Makambako imekuwa ni ya wastani.

Nusu ya mtandao wa barabara za Halmashauri ya Mji ilikuwa inapitika kwa kipindi chote.

Katika kipindi cha Juni 2019 hadi January 2020 ofisi ya TARURA – Katika mji wa Makambako imeendelea na utekelazaji wa kazi za ujenzi wa barabara katika Miradi ya Maendeleo kwa Kiwango cha Lami kilometa 2, Kiwango cha Changarawe Kilometa 10 na Matengenezo ya kawaida ya barabara, Matengenezo ya Muda maalum ya barabara, Matengenezo ya sehemu korofi na ujenzi wa madaraja na makalavati kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kazi zinaendelea na baadhi ya wakandarasi wako site na wengine wamesimama kwa sababu ya mvua.

Mchanganuo wa kazi na matumizi ya fedha umeoneshwa katika Kiambatanisho Na. 1

3. Changamoto katika utekelezaji wa Mipango ya Matengenezo ya barabara

Ofisi ya wakala wa barabara vijijini na mijini inakabiliana na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake.

(a) **Ufinyu wa bajeti**

Ufinyu wa bajeti umesababisha maeneo mengi ambayo ni ya muhimu kutofanyiwa matengenezo ya barabara hasa barabara za mjini na barabara kuu zinazotoka nje ya mji kwenda katika kata za mji na wilaya za jirani, kutokana na kutumika sana hivyo barabara zimekuwa na uharibifu mkubwa hivyo pesa inayotengwa ni finyu kusababisha kutokutosheleza matengenezo hayo. Vilevile eneo la

Mji wa Makambako ni tambarare na linakabiliwa na changamoto ya kukosa mifereji ya maji ya mvua.

(b) **Matumizi mabaya ya miundombinu**

Kumekuwepo na tabia ya baadhi ya wananchi wanaomiliki kundi kubwa la mifugo kupitisha ng'ombe barabarani hususani kata za Kitandililo,Mlowa, Mahongole na Utengule. Pia wananchi wanaomiliki mashamba kuziba mifereji ya kupunguza maji barabarani (Mitre drain) kwa kukwepa maji kuingia katika mashamba yao. Vitendo hivyo vimesababisha miundombinu kuharibika na hata kupelekea barabara kukatika kabisa na serikali kutumia gharama kubwa kurudishia miundombinu hiyo.

(c) **Uchache wa watumishi**

Ofisi ya TARURA- Makambako ina watumishi wanne tu; Wahandisi 2, Fundi sanifu 2. Uchache huu wa watumishi unazorotesha usimamizi wa miradi inayotekelezwa.

4. Hatua Zinazochukuliwa katika Kukabiliana na Changamoto

a. Kuendelea kutoa elimu ya kutunza miundombinu kwa viongozi wa vijiji ili waelimishe wananchi.

b. Kwa kiasi kidogo cha fedha tunachopata tunaendelea kufanya matengenezo maeneo ya barabara yenye uharibifu zaidi.

Naomba kuwasilisha

Eng. Msafiri Abdallah

KAIMU MENEJA WA HALMASHAURI - TARURA

Kiambatanisho Na. 1

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2019-2020) KWA KIPINDI CHA JULAI, 2019 – JANUARY, 2020

A. UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 KWA KUTUMIA FEDHA YA MFUKO WA BARABARA

IBARA	SEKTA/MAELEZO YA ILANI	UTEKELEZAJI ULIOFANIKIWA				
		Na	Jina la mradi	Kazi iliyofanyika	Kiasi cha fedha kilichotumika	% ya utekelezaji/maelezo
1	USAFIRISHAJI NA UCHUKUZI Katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2020 Chama cha Mapinduzi kinaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara na Madaraja	1	Ujenzi wa barabara ya Idara ya maji Mchape,Amani hadi kanisa la sabato kwa kiwango cha Lami km 1	• Kusafisha eneo • Kuondoa tabaka la juu la udongo • Kumalisha tabaka la awali la barabara • Kuweka matabaka mawili • Kuweka lami nyepesi • Kuweka lami nzito • Kuweka kokoto matabaka mawili • Ujenzi wa makalvati mistari miwili • Kuendelea na ujenzi wa mifereji	90,000,000.00	75
		2	Ujenzi wa barabara ya deo sanga hadi A one Lodge kwa kiwango cha Lami km 1	• Kusafisha eneo • Kuondoa tabaka la juu la udongo • Kumalisha tabaka la awali la barabara	0	0

		3	Ukarabati wa barabara ya makambako-Mtanga km10 kwa Kiwango cha Changarawe	• Kusafisha eneo • Kuondoa tabaka la juu la udongo • Kukata na kujaza udongo • Kuumba tuta la barabara km 5.5 • Kufungua mifereji ya kutoa maji katika barabara	32,045,501.00	Kazi imesimama kwa sababu ya mvua.
			JUMLA		**122,045,541.00**	

A. UTEKELEZAJI MIRADI YA MATENGENEZO KWA FEDHA 2019/2020 KWA KUTUMIA FEDHA YA MFUKO WA BARABARA

IBARA	**SEKTA/MAELEZO YA ILANI**	**UTEKELEZAJI ULIOFANIKIWA**				
		Na	**Jina la mradi**	**Kazi iliyofanyika**	**Kiasi cha fedha kilichotumika**	**% ya utekelezaji/maelezo**
		1	Matengenezo ya tahadhari ya barabara za lami za mji wa Makambako.	Maandalizi ya kazi	0	Mkandarasi amekusanya vifaa tayari kwa kuanza kazi
		2	Ujenzi wa madaraja Utengule 1 na utengule II na daraja la Mtimbwe Ngamanga.	• Kusafisha eneo	0	Mkandarasi amesimama kwa sababu ya Mvua.

		3	Matengenezo ya kawaida barabara ya Makambako Mtanga na ujenzi wa daraja la Mtanga.na Daraja la Kifumbe Igongolo.	• Kusafisha eneo la barabara • Kucho barabara kilometa 19 • Kuchimba mifereji ya kutoa maji barabarani	55,400,000.00	Kazi zinaendelea
		4	Matengenezo ya kawaida barabara ya Idofi-Manga, Khanga – Mahongolekm 6, Maeneo korofi Usetule Mbugan km 6.4,Usetule-Idete km4.	• Kusafisha eneo la barabara • Kuchonga barabara km 14	59,013,760.00	Mkadarasi amesimama kwa sababu ya mvua.
		5	Ujenzi wa Daraja la zege Igangidung'u-Mguvani na ujenzi wa Mifereji ya maji Brabra ya Makabeji-Pentekoste.	• Kusafisha eneo • Kuchimba mtaro • Kujenga Mifereji kwa mawe.	22,531,212.00	Mkadarasi amesimama kwa sababu ya mvua.
		6	Matengenezo ya kawaida barabara ya Kiumba-Ngamanga 5km, Matengenezo ya maeneo korofi Ikelu – Mawandekm 3.91, Muungano –	Kazi bado Haijaanza	0.00	Kazi bado Haijaanza

			Utengule km3.96, Ngamanga-Mtimbwe km 4.2 kujaza kifusi daraja la Ikwete Mashujaa.			
		7	Matengenezo ya kawaida barabara ya Makambako S S-Bethsaida 2.85km. and Deo Sanga – A1 Lodge 2.85km ,ujenzi wa makalvati barabara ya Iringa – Range Posta na GOLITHA – Kitisi Makaburini na ujenzi wa mifereji ya maji	• Kuasfisha eneo • Kuchimba mifereji • Kujenga mfereji wa mawe • Kujenga line za makalvati	39,310,800.00	Mkandarasi anaendelea na kazi
			JUMLA		**176,255,732.00**	